# MUHTASARI WA KIKAO MAALUMU CHA BODI YA ZABUNU KILICHOFANYIKA TAREHE 19/1/2022

**MAHUDHURIO:**

| | |
|---|---|
| 1. Ndg RAJABU KHASIMU | Mwenyekiti |
| 2. Ms MAGRETH BUKUKU | Katibu |
| 3. Ndg ADAM SALUM | Mjumbe |
| 4. Ms KULWA MKWAMA | Mjumbe |
| 5. Ndg SAMARA H. MATIKO | Mwanasheria |

SECRETARIETI WALIOHUDHURIA:

1. Happy Mapombe

2. Edwiga Gration

**AGENDA:**

1. Kufungua kikao
2. Kuwasilisha taarifa ya zabuni mbalimbali
   - Ujenzi wa nyumba ya watumishi katika hospitali ya wilaya zabuni Na. LGA/033/2021/2022/W/36/lot 2
   - Ujenzi wa **ICU** katika Hospitali ya wilaya Karagwe zabuni Na. LGA/033/2021/2022/W/36/lot 1
   - Zabuni ya usafi na uzoaji taka ngumu maeneo ya Kayanga na Omurushaka zabuni Na LGA/033/2021/2022/NCS/4 LOT 1
   - Zabuni ya usafi makao makuu zabuni Na LGA/033/2021/2022/NCS/4 LOT 2

3 . Kufunga kikao

**Kumb. NA 14/2022/23/ 1 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwakaribisha wajumbe wa bodi ya zabuni pamoja na Secretariet ya Manunuzi kwenye kikao maalum cha Bodi ya Zabuni. Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa kikao hiki kinagusa mradi wa Ujenzi wa ICU, Nyumba ya watumishi na usafi wa mazingira na uzoaji wa takangumu. Alieleza kuwa miradi hii inahitaji kujadiliana kwa makini ili kupata mwelekeo utakao leta tija kwenye Taasisi. Aidha Mwenyeketi alimweleza Katibu kufuatilia posho za vikao vya Bodi kwa Mkurugenzi mtendaji. Mwenyekiti alieleza kwa masikitiko kuwa vikao vingine vinafanyika kwenye tasisi hii vinalipwa na wakati bodi inadai vikao vingi vya nyuma. Baada ya utangulizi huo Mwenyekiti alifungua kikao saa 3.00 kamili asubuhi.

**15/2022/23/ 1 *UJENZI* <u>WA NYUMBA YA WATUMISHI KATIKA HOSPITALI YA WILAYA ZABUNI Na. LGA/033/2021/2022/W/36/LOT 2</u>**

Taarifa ya manunuzi iliwasilishwa ikieleza kuwa mradi wa ujenzi wa nyumba ya watumishi ulitengewa bajeti ya Tsh. 90,000,000.00. Mchakato wa kumpata Mkandarasi ulifanyika kwa njia ya single source ambapo SUMA JKT alipewa kabrasha la zabuni ambalo alilijaza na kulirudisha Halmashauri ya wilaya ya Karagwe tarehe 24/12/2021. Kabrasha lilifunguliwa mzabuni alionyesha kuifanya kazi hii ya ujenzi kwa gharama ya **Tsh191,868,940/=.**Taarifa ya menejimenti ya ununuzi wa umma ilieleza kuwa kamati ya taathmini iliundwa na Mkurugenzi Mtendaji ikiwa na wajumbe wanne ambao ni:

| | |
|---|---|
| 1.NTENGWA L.MADUHU | Mwenyekiti |
| 2.DIDACE NJONDI | Katibu |
| 3.JIMMY NJAU | Mjumbe |
| 4.PONSION KATABARO | Mjumbe |

Taarifa ya menejimenti ya ununuzi illieza kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi na matokeo ya tathmini yalionyesha kuwa gharama zilizowasilishwa zilikuwa kubwa kuliko bajeti ya Halmashauri hivyo , kamati ilishauri kazi hii irudiwe. Taarifa ya menejimenti ya manunuzi (PMU) ilielezea kuwa kupitia kanuni ya 220(2) ya mwaka 2013 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016 ilipitia taarifa iliyowasilishwa na kamati ya tathmini na kukubaliana na ushauri wa kuirudia kazi hii. Aidha taarifa ya PMU ilieleza kuwa ilipokelewa barua yenye kumb Na: AH. 161/298/01 ya tarehe 13/1/2022 kutoka TAMISEMI ambayo ilitoa maelezo kuwa imebaini kuwa Halmashauri nyingi Tanzania zimeshindwa kumpata mkandarasi mwenye bei ambazo ziko ndani ya bajeti hivyo ilitoa mwongozo wa kutumia Force akaunti. Taarifa ya PMU ilieleza kwamba muda uliotolewa na TAMISEMI ni mfupi hivyo iliombwa ridhaa ya kuifanya kwa njia ya single source kwa kuipatia Taasisi ya serikali ambayo ni Magereza.

Wajumbe wa bodi walijadili taarifa hii kwa kina hawakukubaliana na ushauri wa PMU kwa maelezo kuwa kazi hii ina vitu vinavyohitaji utaalam(complex) hivyo walitia shaka utendaji wa kazi wa taasisi hiyo.

AZIMIO: Wajumbe waliazimia kuwa kazi hii ifanyike kwa njia ya ushindani na ofisi ya magereza wahusishwe.

**Kumb. NA 16/2022/23/ 1 <u>UJENZI WA ICU KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA KARAGWE</u>**

Taarifa PMU ilieleza kuwa ina maelezo sawa na maelezo yaliyoko kwenye ujenzi wa nyumba ya watumishi tofauti ni bajeti ya ujenzi ilikuwa sh. 300,000,000/= na mzabuni aliwasilisha sh. 324,867,000/= hivyo kamati ya tathmini ilitoa ushauri kazi irudiwe.

Taarifa ya PMU ilitoa ushauri kwa bodi ya zabuni kuwa kazi hii kutokana na uharaka ifanyike kwa single source kwa kuipa ofisi ya magereza.

Wajumbe wa Bodi baada ya kujadiliana kwa kina hawakukubaliana na ushauri uliotolewa na PMU kwa maelezo kuwa hawajawahi kuona magereza ya Kayanga ikifanya miradi mikubwa inayolingana na kazi inayotaka kutolewa.

MAAZIMIO: Wajumbe waliazimia kwamba kazi ya kumpata fundi itangazwe na kazi ya ununuzi wa vifaa izingatie mwongozo wa force akaunti.

**Kumb. NA 17/2022/23/1 ZABUNI YA USAFI NA UZOAJI TAKA MAENEO YA KAYANGA NA OMURUSHAKA**

Taarifa ya PMU iliwasilishwa ikieleza kuwa zabuni hii ilitengewa bajeti ya Tsh. 25,800,000/= kwa miezi sita. Mchakato wa manunuzi ulifanyika na yalijitokeza makampuni mawili ambayo yalionyesha nia ya kuchukua na yalirudisha na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:

| Jina la Mzabuni | Kiasi kwa mwezi | Kiasi kwa mwaka |
|---|---|---|
| BUGOMBE COMPANY | 5,000,000.00 | 60,000,000.00 |
| RAM INVESTMENT COMPANY LTD | 9,500,000.00 | 114,000,000.00 |

Taarifa ya manunuzi ilieleza kuwa kamati ya tathmini iliundwa na watu wanne ambao ni:

| | |
|---|---|
| 1. FLORIAN OSWARD | Mwenyekiti |
| 2. HAPPINESS MAPOMBE | Katibu |
| 3. GERALD LWEYO | Mjumbe |
| 4. PETER EVALISTER | Mjumbe |

Taarifa ya tathmini ilionyesha mzabuni BUGOMBE Company alikuwa mzabuni ambaye ameweka kiwango cha chini cha pesa. Taarifa ya menejimenti ya manunuzi inaeleza kuwa kamati ya tathmini haikumpitisha kwa kuwa kiwango chake kilizidi bajeti ya Halmashauri hivyo kamati ilipendekeza mtoa huduma asipewe kazi ya usafi na uzoaji taka katika mji wa Kayanga na Omurushaka badala yake kazi irudiwe. Taarifa ya PMU iliwasilishwa ikieleza kuwa ilikubaliana na mapendekezo ya kamati ya tathmini na kutoa ushauri kwa bodi ya zabuni kama ifuatavyo:

Kwa kuwa kuna kipengele cha 9 cha mkataba wa usafi na uzoaji taka kwa mwaka 2021/2022 kinaruhusu mkataba kuafanyiwa marekebisho hivyo PMU inashauri mkataba huu ufanyiwe marekebisho kwenye maeneo yafuatayo

Kifungu no 2 : Juu ya kiasi cha mkataba ambacho kinasomeka sh. 4,300,000/= badala yake kiandikwe gharama ya mkataba ni 4,264,000/= hii imetokana na kwamba hesabu zilikosewa kujumlishwa.

- Kutokana na kukosewa kwa ukokotoaji wa hesabu kumepelekea tofauti ya Tsh. 36,000/=. Gharama hizi mzabuni atapaswa kuzirudisha Halmashauri . Mzabuni hadi sasa amefanya kazi miezi 18 hivyo atadaiwa kiasi cha sh. 18 x 36000=648,000/=
- Kiongezwe kipengele kwenye mkataba kinacholazimu malipo ya wakala kulipwa kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa kazi(certificate) kwa kila siku ambao utajumlishwa kwa mwezi.
- Kubadili kipengele namba 4 cha mkataba juu ya tarehe ya kuanza mkataba na kumaliza mkataba ambapo sasa kwenye mkataba wa nyongeza utasomeka tarehe ya kuanza mkataba ni tarehe 1/1/2022 na tarehe ya kumaliza mkataba nia tarehe 30/6/2022.
- Majadiliano yafanyike ili kukubaliana na mtoa huduma wa usafi na uzoaji taka juu ya mabadiliko haya. Aidha timu ya majadiliano itapitia baadhi ya vipengele ambavyo vinaleta utata ili kusahihisha. Kwa mfano

kifungu Na 6 kinaeleza mtoa huduma anapaswa kulipwa ndani ya siku thelathini (30) tangu alipoanza kufanya kazi. Kifungu hiki hakitekelezeki kwa kuwa makubaliano ni kulipwa kwa mwezi . Kumlipa mzabuni ndani ya siku 30 ina maanisha mwezi utakuwa haujakamilika.

- Kuongeza kiambatishi cha masharti ya Jumla ya mkataba (General Condition of Contract) na mashart maalum ya zabuni (Special condition of Contract)

Uwepo wa Kiambatishi hiki kinasaidia katika mazingira mbalimbali yanayojitokeza wakati wa utekelezaji wa mkataba kwa mfano yanapotokea mazingira ya kumwongezea mtoa huduma muda wa mkataba (extension time ). Afisa masuhuri kupitia sheria ya manunuzi ya mwaka 2011 kanuni ya 111(1) ya mwaka 2013 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016 ina mruhusu kumwongezea muda wa mkataba mtoa huduma lakini kanuni ya 111(2) ina mlazimu Afisa masuhuri kumwongezea mkataba mtoa huduma kwa kurejea masharti ya Jumla ya Mkataba (General Condition Of Contract) nanukuu "An order for extension of time may be issued only by the accounting officer. The order shall state the section of the general condition of Contract under which it is issued"

Nyongeza za muda zilizofanyika kwa mtoa huduma Nassoro Seleman Maharuq zilifanyika bila kutaja kifungu cha mashart ya jumla ya mkataba kama sheria ya manunuzi inavyo elekeza hii inatoka na sababu kuwa, kutoka mwanzo kiambatishi hiki hakikuwekwa kwenye mkataba .Kutokuwepo kwa kiambatishi hiki kwenye nyongeza ya mkataba unaotaka kufanyika sasa kutapelekea Halmashauri kupata hoja ya manunuzi endapo ita mwongezea muda wa kazi ,kwakuwa nyongeza hiyo itakuwa inakiuka sheria ya manunuzi inayo lazimu nyongeza itokane na masharti ya Jumla ya mkataba .

Baada ya kupitia taarifa ya PMU wajumbe walijadiliana na kisha walimuuliza katibu ni kwanini kazi hii isirudiwe sasa badala ya kumuongezea mkataba wa nyongeza wakala aliepo ! Katibu alitoa ufafanuzi kuwa kazi hii imerudiwa mara mbili inakosa wazabuni kwa kigezo kuwa gharama zinakuwa juu ya bajeti ya Halmashauri kwa hiyo inaonekana kiwango kilichotengwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hakikuzingatia bei ya soko. Aidha katibu alieleza kuwa bajeti ijayo 2022/2023 kiwango cha fedha ya usafi kimeongezwa hivyo PMU imeonelea kwa kipindi hiki ambacho bajeti ni finyu mzabuni aliyepo aendelee kufanya usafi ili kumalizia kipindi hiki cha mpito. Katibu wa bodi ya zabuni aliwaeleza wajumbe kuwa tunalazimika kumuongezea muda mzabuni aliyepo kwa sababu muda uliobaki kumalizia bajeti 2021/2022 ni takribani miezi mitano.

Mchakato wa kumpata mzabuni kwa kutumia muda wa kila hatua uliowekwa kwenye sheria ya manunuzi katika marekebisho ya mwaka 2016 itachukua siku zisizopungua 90 hivyo mtoa huduma atakayepatikana atalazimika kufanya kazi kwa miezi miwili na kuifanya PMU ianze kuchakata tena kumtafuta mtoa huduma wa usafi kwa bajeti ya 2022/2023 jambo ambalo ni usumbufu kwa mzabuni atakayekuwa ameshinda zabuni na pia Halmashauri itaingia gharama za mchakato wa zabuni.

Baada ya maelezo hayo yaliyotolewa na katibu wa bodi ya zabuni wajumbe walikubaliana na ushauri uliotolewa kwa kumuongezea wakala muda wa mkataba.

AZIMIO 1: Wajumbe waliazimia mtoa huduma aongezewe mkataba kuanzia tarehe 1/1/2022 hadi tarehe 30/6/2022

AZIMIO 2: Wajumbe waliazimia wakala aitwe kwenye majadiliano ili kupata nyongeza ya mkataba ambao una makubaliano ya pande zote mbili.

**Kumb. NA 18/2022/23/1 <u>ZABUNI YA USAFI MAKAO MAKUU YA WILAYA(HEAD QUARTER)</u>**

Taarifa ya menejimenti ya ununuzi wa Umma iliwasilishwa ikieleza kuwa zabuni hii ilitolewa kwa kotesheni na kufanyiwa tathmini. Matokeo ya tathmini yalionyesha mshindi ataifanya kazi hii kwa sh. 1,300,000/=. Kamati ya tathmini iliridhia mtoa huduma Safe Gain Company Limited ambaye alikuwa ametimiza vigezo na alikuwa na bei ya chini apewe kazi ya usafi katika ofisi za Halmashauri pamoja na mazingira ya nje. Taarifa ya PMU iliwasilishwa ikieleza kuwa ilikubaliana na ushauri uliotolewa na kamati ya tathmini lakini ilitoa ushauri kwa bodi ya zabuni kuwa mzabuni huyu asipewe kazi hii kwa kuwa bajeti iliyokuwa imetegemewa kutumika ilishatumiwa kwenye idara ya utawala kwa kununua vifaa vya usafi.

Wajumbe wa bodi baada ya kujadiliana na kubaini kuwa kazi hii ya usafi haina bajeti iliridhia kazi hii isitishwe isubiri bajeti ya 2022/2023.

AZIMIO: Wajumbe wote wa bodi ya zabuni walikubaliana kazi hii itengewee fedha kwenye bajeti ijayo baada ya kupata uhakika PMU ndipo ifanye mchakato wa kuirudia.

**Kumb. NA 19/2022/23/1 KUFUNGA KIKAO**

**Mwenyekiti alifunga kikao saa 6.10 mchana.**

**UMETHIBITISHWA**

..............................

..............................

**(Magreth Bukuku)**

**KATIBU**

**(RAJABU Khasimu)**

**TAREHE** 19.01.2022

**MWENYEKITI**

## YATOKANAYO NA KIKAKO MALUUM CHA BODI YA ZABUNI CHA

## TAREHE 19/1/2022

| S/N | AZIMIO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | Wajumbe waliazimia mtoa huduma aongezewe mkataba kuanzia tarehe 1/1/2022 hadi tarehe 30/6/2022 | Agizo limezingatiwa .rasimu ya mkataba wa nyongeza imeandaliwa itawasilichwa kwenye kikao cha bodi ya zabuni kwa ajili ya kupitia na kuridhia mabadiliko ya mkataba |
| 2 | Wajumbe waliazimia wakala aitwe kwenye majadiliano ili kupata nyongeza ya mkataba ambao una makubaliano ya pande zote mbili. | Majadiliano yalifanyika taarifa itawasilishwa kwenye kikao |